

**MEZA YA BWANA**  
**KRISTO ALITUKOMBOA NA LAANA YA TORATI**  
**GAL. 3: 13 – 14, KUMB. 21: 23**

**1. Laana ki-Ebrania ilikuwa ni mamlaka iliyokuwa inafungulia nguvu Fulani mbaya ili impate mtu fulani ambaye ametenda dhambi, au ameasi juu ya amri za Mungu au amewadharau wazazi wake waliomzaa.**

- Ni kiziwi peke yake katika Torati ambaye hakuruhusiwa kulaaniwa maana alikuwa hana uwezo wa kusikia tangazo la hukumu hiyo. **Lawi 19: 14**
- Kwa hiyo hali aliyoipata Yesu Kristo pale msalabani wakati anasulubiwa; ile hali ya kuzomewa hovyoy, kuteswa hovyoy, kutoa jasho hadi damu, kukataliwa na watu wake na kuonekana kama kinyaa katika jamii, kuaibishwa na hatimaye kufa kifo cha aibu; hiyo ndiyo picha halisi ya mtu aliyelaaniwa – ki-Ebrania; **na ndiyo sababu Yesu aliomba sana ili kikombe hiki kimwepuke. Math 26: 38 – 45.**
- Hiyo ndiyo ilikuwa haki yetu sote tangu Adamu na Hawa **walipoasi** amri ya Mungu wetu pale bustani ya Edeni na Mungu kutangaza laana juu yao (Hukumu) na baadae kuwafukuza kabisa katika bustani ya Edeni nzuri ajabu aliyokuwa amewatengenezea. **Mwanz 3: 9 – 24.** Huu ulikuwa ndiyo mwanzo wa Mungu kufungulia nguvu mbaya ili iwatese Adamu na Hawa na kuwafanya wasiwe na Amani wala furaha tena katika maisha yao ya ndoa na hata watoto wao watakaowazaa baadae.

## **2.A.Torati inaorodhesha aina mbalimbali za laana kama vile *Kumb: 27: 15 – 26 Tusome***

**B.**Torati inaenda mbali zaidi pale zinapoorodheshwa laana zitakazompata mtu ambaye atakataa kusikiliza sauti ya Mungu na kukaidi kufanya maagizo ya Bwana. ***Kumb 28: 15 – 49 (Tusome wote)***

- kwa hiyo mtume Paulo anaposema wazi kwamba Yesu Kristo alituokoa na laana ya torati; alikuwa anamaanisha jambo kubwa sana ambalo Kristo alilifanya pale msalabani kwa niaba yetu. ***Isaya 53: 1 – 12 (Luka 23: 33 – 49, Math 27: 27 – 54)***. Furaha yetu, amani yetu, siyo kwa sababu tuna fedha, dhahabu, nyumba, magari n.k. Furaha yetu inatokana na Yesu kulipa deni hili kubwa la dhambi zetu na kufanya tuhesabiwe haki bure mbele za Mungu Baba na kuifuta kabisa ile hati ya mashitaka yaliyokuwa yanatukabili. **Kol. 2: 13 – 15.**

3. Tunaposhiriki meza ya Bwana leo; tunatangaza wazi kuwa Kristo ametukomboa na **laana ya Torati** ametukomboa na matangazo yote ya laana yaliyotolewa juu yetu na **shetani** mwenyewe; **mababu zetu, mabibi zetu** na mapepo yote!! Laana ya magonjwa sugu, mikosi kutofanikiwa, mateso, kufa hovyoyote, kuonekana kama kinyaa katika jamii, ajali za hovyoyote, vyote hivi kwa sasa **havituhusu** sisi wateule wa Mungu; Yesu alilaaniwa kwa niaba yetu na kisha akafuta hati zote za laana dhidi yetu. ***Kolos 1: 13 – 23, 2: 10 – 15.***

- Kamwe kwa sasa laana ya torati siyo haki yetu na laana isiyo na sababu haitupati ng'oo!! ***Mith 26: 2***
- Lakini zaidi sana shetani hana uwezo tena wa kutulaani maana sisi ni wabarikiwa na tuna mafuta ya Bwana juu yetu. ***Hesab 22: 12 na 1Samwl 17: 40 – 51. Amina***

**Na**

**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**

**17/01/2021**